# Mwongozo wa Wazazi: Tathmini Mbadala ya Kentucky: Maneno Muhimu ya Kujua na Maswali na Majibu

***Ilipitiwa tena Oktoba 2024***

Madhumini ya *Mwongozo wa Wazazi: Tathmini Mbadala ya Kentucky (Alternate Kentucky Summative Assessment (AKSA))* ni kutoa maneno muhimu na kujibu maswali ambayo huenda wazazi wanayo kuhusu Tathmini Mbadala ya Kentucky ili waweze kufanya maamuzi kuhusu mtoto wao baada ya kuarifiwa.

## Maneno Muhimu ya Kujua

**Marekebisho:** Kubalisha vifaa au taratibu zinazomsaidia mwanafunzi kujifunza na kufanya tathmini. Marekebisho hayabadilishi maudhui au madhumuni ya somo linalofundishwa au kutathminiwa. Marekebisho ya tathmini yanakusudiwa kumruhusu mwanafunzi kufanya tathmini na kupata matokeo halali yanayoonyesha mambo ambayo mwanafunzi anajua na anaweza kufanya.

**Kurekebisha Mafundisho:** Mabadiliko yanayolingana na mahitaji mahususi ya mwanafunzi. Kubadilisha nyenzo zilizopo au mbinu ya kufundisha ili kukidhi mahitaji ya mwanafunzi. Mifano ni pamoja na vielekezi vya kichwa, ishara za mawasiliano ya picha (Mayer Johnson), picha, kuweka vielekezi pamoja na vitu halisi, vitu halisi, picha zilizoongezewa ukubwa, picha zinazoweza kuonekana vizuri zaidi, kutumia rangi zinazoweka kuonekana vizuri zaidi au lugha ya ishara za kusaidia mtu kwa kusogeza mikono yake.

**Uwezo wa Kufanya Shughuli za Kila Siku:** Shughuli muhimu ambazo mtu anahitaji kufanya ili aweze kuishi kwa kujitegemea na kwa usalama katika maisha ya kila siku.

**Kamati ya Uandikishaji na Ukaguzi (Admissions and Release Committee (ARC)):** Timu ya watu binafsi ambayo hufanya maamuzi ya elimu kwa ajili ya mtoto anayehitaji elimu maalum. Inajumuisha mzazi, mtoto (kama inavyofaa), mwalimu(walimu) wa elimu ya kawaida, mwalimu(walimu) wa elimu maalum, mwakilishi wa wilaya (mwalimu mkuu, mkurugenzi wa elimu maalum, mshauri, nk), watathmini na watoa huduma wa huduma zinazohusiana.

**Viwango Mbadala vya Mafanikio:** Kiwango mbadala cha mafanikio huweka matarajio ya utendaji ambayo huwa tofauti na kiwango cha mafanikio ya darasa husika. Kwa ujumla, viwango mbadala vya mafanikio lazima vilingane na viwango vya maudhui ya masomo ya jimbo, vimsaidie mwanafunzi kujifunza kwa kutumia mtaala wa jumla na vionyeshe kuwa uamuzi wa viwango vya juu zaidi vya mafanikio ulifanywa. [Tazama34 C.F.R. §200.1(d)]

**Lengo la Tathmini Mbadala:** Lengo linawakilisha vikwazo vya Kiwango cha Masomo cha Kentucky (Kentucky Academic Standard (KAS)). Lengo la Tathmini Mbadala linaweza kupunguza sehemu za kiwango kwa kuzingatia mwongozo maalum kuhusu jambo ambalo kipengee cha tathmini kinaweza kuwakilisha. (Viwango vya Masomo vya Kentucky - KSA Mbadala 2023)

**Cheti Mbadala cha Shule ya Upili:** Hutolewa kwa wanafunzi wenye ulemavu ambao hawawezi kukidhi mahitaji ya kupa cheti cha kawaida cha shule ya upili. Wapokeaji wa cheti mbadala cha shule ya upili watafanya tathmini mbadala na kukamilisha kozi mbadala ya kujifunza. Cheti mbadala cha shule ya upili si sawa na cheti cha kawaida cha shule ya upili.

**Teknolojia ya Kusaidia:** Zana na mikakati inayotumiwa kusaidia wanafunzi kufanya maendeleo na kushiriki ipasavyo katika masomo, mahusiano ya kijamii na shughuli za ajira; inaweza kuwa teknolojia ya chini (kwa mfano, mifumo ya mawasiliano isiyohitaji vifaa vingine, lugha ya ishara, nk) hadi teknolojia ya juu, kama vile kompyuta zilizo na vifaa vya kuunganishwa kwa swichi.

**Shughuli za Kupima Ujuzi:** Matukio ya kutekeleza shughuli zinazohitaji wanafunzi wakamilishe shughuli, huku wakifanya kazi hatua kwa hatua, kama walivyoelekezwa na mwalimu.

**Zana na Mikakati Mbadala ya Kusaidia katika Mawasiliano (Augmentative and Alternative Communication (AAC))**: Mfumo wa teknolojia ya chini, ya kati au ya juu ambayo husaidia mwanafunzi katika lugha ya kujieleza (kwa mfano, kuomba kitu, kuuliza na kujibu maswali, kuelezea mambo au matukio na kukataa, vifaa vya kutoa sauti kama vile vifaa vya kusaidia katika kugeuza maandishi kuwa usemi, picha au bodi za ishara).

**Uwezo wa Kuwasiliana**: Kutumia mfumo wa mawasiliano ambao unawawezesha wanafunzi kukuza na kuonyesha ujuzi.

**Malengo ya Maudhui:** Viwango vya maudhui vinavyozingatiwa katika tathmini. Katika Tathmini Mbadala ya Kentucky (Alternate Kentucky Summative Assessment (AKSA)), malengo ya maudhui yanazingatia Shughuli za Kupima Ujuzi kulingana na ngazi ya darasa katika kusoma, hisabati, sayansi, masomo ya kijamii na kuandika.

**Data ya Sasa:** Data zilizokusanywa ndani ya kipindi cha hivi majuzi cha siku 365. Mifano ni pamoja na data ya ufuatiliaji wa maendeleo ya IEP, ripoti za maendeleo ya IEP, tathmini za darasa, uchunguzi wa darasa, mifano ya kazi, data ya tathmini ya tabia, tathmini za mpito, tathmini za teknolojia ya kusaidia na rekodi za mahudhurio.

**Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner (EL)):** EL ni mwanafunzi ambaye lugha yake ya asili ni lugha nyingine ambayo si Kiingereza au mwanafunzi anayetoka katika mazingira ambapo lugha nyingine ambayo si Kiingereza huathiri sana kiwango cha ustadi wa lugha ya Kiingereza cha mtu binafsi. Matatizo ya EL ya kuzungumza, kusoma, kuandika au kuelewa lugha ya Kiingereza yanaweza kumzuia kujifunza katika madarasa yanayofundishwa kwa Kiingereza na kufanya tathmini zilizowasilishwa kwa Kiingereza.

**Sheria ya Kuhakikisha kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu (Every Student Succeeds Act (ESSA):):** Mnamo Desemba 2015, Bunge la Marekani liliidhinisha tena Sheria ya Elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari (ESEA), sheria kuu ya shirikisho inayoongoza elimu ya umma ya wanafunzi wa chekechea-darasa la 12. Sheria inayojulikana kama Sheria ya Kuhakikisha kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu (ESSA), ilichukua nafasi ya Sheria ya Kuboresha Masomo ya Wanafunzi Wote (No Child Left Behind (NCLB)) na kuunda sera ya muda mrefu inayowapa majimbo fursa za kubadilika zaidi kulingana na hali na uwezo wa kudhibiti zaidi mchakato wa uwajibikaji. (Idara ya Elimu ya Marekani)

**Uthibitisho:** Huu unarejelea vyanzo mahususi vya taarifa vinavyotumiwa kutambua sifa za mwanafunzi ambazo zinakidhi au hazikidhi vigezo vya ushiriki.

**Inazidi Marekebisho:** Marekebisho, mabadiliko na teknolojia saidizi ambayo INAZIDI kinachoruhusiwa kwenye tathmini ya jumla ya wanafunzi, kama ilivyoelezwa katika

Ujumuishaji wa Watu Wanaohitaji Huduma Maalum katika Mipango ya Tathmini Zinazohitajiji na Jimbo na Uwajibikaji na ilivyoandikwa katika 703 KAR 5:070.

**Mafundisho ya Moja kwa Moja ya Mtu Binafsi:** Mafundisho yanayotumia mbinu mbalimbali yaliyoundwa kwa ajili ya mwanafunzi binafsi. Wanafunzi wenye matatizo makubwa ya utambuzi wa akili huhitaji aina hii ya mafundisho ili waweze kukuza ujuzi na stadi zinazozingatia muktadha. Wanafunzi wenye matatizo makubwa ya utambuzi wa akili wana uwezekano mkubwa wa kuhitaji aina hii ya mafundisho sana ili waweze kutumia ujuzi na stadi katika mazingira mengi.

**Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)):** Sheria ya shirikisho iliyotungwa mnamo mwaka 1990 na kuidhinishwa tena mnamo mwaka 1997 na tena mnamo mwaka 2004. Imeundwa ili kulinda haki za wanafunzi wenye ulemavu kwa kuhakikisha kuwa kila mtu anapata elimu ya umma bure (FAPE), bila kujali uwezo. Lengo la IDEA si tu kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye ulemavu wanapata fursa sawa bali pia ni kutoa huduma za ziada za elimu maalum na utaratibu wa kulinda haki.

**Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi Individual Education Program (IEP)):** Umeandikwa ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya mtoto aliyetambuliwa kuwa na ulemavu. Ni makubaliano ya kisheria ambayo huhakikisha kuwa mtoto atapata huduma zilizobainishwa katika mpango.

Mwongozo wa Kutengenza IEP hutoa maagizo na mifano ya kutengenza IEP.

**Viwango vya Masomo vya Kentucky (Kentucky Academic Standards (KAS)):** Ni viwango vya chini zaidi vinavyohitajika yaani wanafunzi wote wa Kentucky wanapaswa kuwa na fursa ya kujifunza kabla ya kuhitimu kutoka shule za upili za Kentucky. Viwango vinazungumzia mambo ambayo wanafunzi wanapaswa kujifunza, lakini havizingumzii jinsi ambavyo uzoefu wa kujifunza umeundwa au rasilimali zinazopaswa kutumiwa. Viwango husaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wote huko Kentucky hufunzwa maudhui ya kawaida na wana fursa za kujifunza katika ngazi za juu.

**Fomu ya Taarifa ya Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky:** Fomu inabainisha mahitaji ambayo mwanafunzi lazima atimize ili aweze kufanya tathmini mbadala. Mahitaji haya lazima yakubaliwe na ARC na kupitiwa tena katika mkutano wa kila mwaka.

**Maendeleo ya Kujifunza:** Maelezo kuhusu jinsi ambavyo wanafunzi wanaokua wanaweza kukua na kukuza satdi za masomo baada ya muda. Maendeleo ya kujifunza yanaweza kuwa zana muhimu kwa walimu wakati wa kubaini hatua ya mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza stadi maalum au kuelewa dhana.

**Zana ya Sifa za Wanafunzi (Learner Characteristics Inventory (LCI)):** Hojaji inayomsaidia mwalimu kuelewa uwezo wa kipekee wa kila mwanafunzi katika nyanja mbalimbali: mawasiliano ya kujieleza, mawasiliano ya kusikiliza, kusikia, kuona, mwendo wa misuli, kushiriki, mahudhurio, stadi za kusoma na stadi za hisabati. LCI ina madhumuni mawili ya msingi: 1) kuelezea sifa mbalimbali za wanafunzi wanaofanya tathmini mbadala na 2) kuelezea kiwango ambacho mifumo ya sifa hizo zilijitokeza ndani ya na kote katika jimbo.

**Data ya Muda Mrefu:** Data ambazo zimekusanywa na kuchambuliwa kwa muda mrefu na zaidi ya mwaka mmoja. Seti ya data inachukuliwa kuwa ya muda mrefu ikiwa inafuatilia aina sawa ya taarifa kuhusu washiriki sawa katika kipindi vingi vya wakati. Mifano ya data ya muda mrefu ni pamoja na Historia ya Maendeleo ya Jamii, ripoti za tathmini jumuishi, tathmini za utambuzi, matokeo ya tathmini ya jimbo na wilaya, vipimo vya shughuli za kila siku, data ya ufuatiliaji wa maendeleo, data ya tathmini ya tabia, tathmini ya mpito na tathmini ya teknolojia.

**Njia ya Mawasiliano:** Njia kuu ambayo mwanafunzi hutumia kuelezea mawazo yake, kama vile kupitia maneno, picha, vitu, vidokezo vya kugusika na teknolojia ya mawasiliano/teknolojia ya kusaidia.

**Mabadiliko:** Kubadilsiha nyenzo au taratibu wakati wa mafundisho na tathmini ambako hubadilisha matarajio ya kujifunza ya maudhui ya kiwango cha darasa. Huenda mabadiliko wakati wa mafundisho yakafaa kwa muda mfupi kwa ajili ya kukuza uelewa na stadi za mwanafunzi. Unapaswa kuepuka mabadiliko ya tathmini kwa sababu huwa ni njia mbaya ya kupima ujuzi na stadi za mwanafunzi.

**Hakuna Mtoto Anayeachwa Nyuma:** Sheria ya shirikisho iliyopitishwa mnamo mwaka wa 2002 ili kuhakikisha kuwa shule za msingi na za sekondari zinawajibika kwa viwango vya juu kwa njia inayoweza kupimika. NCLB inahitaji asilimia 100% ya wanafunzi (ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa elimu maalum na wanaotoka katika mazingira yaliyowazuia kukuza ujuzi unaohitajika) katika shule wafikie seti sawa ya viwango vya jimbo katika hisabati na kusoma ifikapo mwaka wa 2014. NCLB ilibadilishwa na Sheria ya Kuhakikisha kuwa Kila Mnafunzi Anafaulu (ESSA) mnamo mwaka wa 2015.

**Vigezo vya Kushiriki:** Maelezo haya hutoa taarifa zaidi juu ya sifa za wanafunzi ambazo wanafunzi wahitajika ili wakidhi vigezo vinne vya kushiriki katika tathmini mbadala.

**Mafundisho Yanayohitajika:** Yanapatikana katika nyanja za maudhui ya masomo na katika mazingira mengi (ikiwa ni pamoja na shule, nyumbani na jamii).

**Mafundisho Yaliyoundwa kwa Njia Maalum (SDI):** Kubadilisha maudhui, mbinu au mbinu ya kufundisha ili kushughulikia mahitaji ya mtu binafsi ya mtoto na kuhakikisha kuwa anajifunza kwa kutumia mtaala ili mtoto aweze kutimiza viwango vya elimu vilivyowekwa.

**Vipengee vya Majibu Vilivyoteuliwa:** Vipengee vya tathmini ambavyo vimeundwa ili wanafunzi wajibu kwa kuchagua jibu (kwa mfano, machaguo mengi, kweli au uongo).

**Usaidizi Mwingi:** Unajumuisha usaidizi kutoka kwa walimu na watu wengine (kwa mfano, mwalimu wa rasilimali, mwalimu mwenza, msaidizi) na usaidizi mbalimbali wa nyenzo kayika mazingira ya mwanafunzi. Mifano ni pamoja na kubadilisha maandishi kulingana na tathmini na mafundisho na mbinu ya kufundisha kwa kutoa usaidizi wa muda ili mwanafunzi ajifunze mambo mapya.

**Vifaa Vilivyobadilishwa kwa Kiasi Kikubwa:** Vifaa vilivyobadilishwa kwa kiasi kikubwa ni pamoja na darasa mbalimbali na vifaa vingine ambavyo muonekano wao umebadilishwa na maudhui ya nyenzo ambazo warika zake wasio na ulemavu hutumia kujifundisha au kufanya tathmini.

Mifano ni pamoja na kufupisha urefu wa vifungu kwa kiasi kikubwa au kutumia nukta zilizoinuliwa na kuhesabu kwa kusogeza mkono wake wakati wa kutambua nambari inayolingana katika hisabati.

**Tathmini ya Kusoma, Hisabati na Sayansi (Transition Attainment Record (TAR):** Orodha ya ukaguzi ambayo hutathmini ikiwa mwanafunzi amekuza stadi za kusoma, hisabati na sayansi.

## Maswali Yanayoulizwa Sana

1. **Je, Tathmini Mbadala ya Kentucky (Alternate Kentucky Summative Assessment (AKSA)) ni nini?**

   AKSA (hapo awali ilijulikana kama K-PREP Mbadala) hufanywa na wanafunzi wenye ulemavu mkubwa zaidi wa utambuzi wa akili. Huenda wanafunzi wenye ulemavu huu wakahitaji njia mbadala ya kushiriki katika tathmini ya jimbo la Kentucky ili kuonyesha kuwa wamefaulu. Tathmini mbadala imeundwa ili kushughulikia mahitaji ya wanafunzi kwa kuruhusu kubadilisha mafundisho, mabadiliko na njia mbadala za kushiriki katika tathmini ya jimbo.

   Taarifa Zaidi:

   Ukurasa wa wavuti wa Tathmini Mbadala ya Kentucky

2. **Je, nani anatathminiwa?**

   Kila mwanafunzi katika darasa la 3 hadi 12 hufanya tathmini ya viwango mahususi katika ngazi mbalimbali za darasa. Kuna wanafunzi wenye ulemavu ambao hufanya Tathmini Mbadala ya Kentucky (Kentucky Summative Assessment (KSA)) bila marekebisho na wengine hufanya tathmini kwa marekebisho. Wanafunzi ambao wametambuliwa kuwa na ulemavu mkubwa wa utambuzi wa akili na wanaokidhi Miongozo ya Kufanya Tathmini Mbadala ya Kentucky watafanya tathmini mbadala inayoitwa AKSA.

   Taarifa Zaidi:

   Taarifa kuhusu ni masomo yanayojaribiwa katika kila ngazi ya darasa kwa wanafunzi wanaofanya tathmini mbadala imewekwa kwenyeukurasa wa wavuti wa Tathmini Mbadala ya Kentucky .

3. **Je, wanafunzi wa ngazi gani za madarasa hutathminiwa katika AKSA?**

   Tathmini mbadala ina vipengele viwili vikubwa:

   - Shughuli za Kupima Ujuzi ambazo hupima utendaji wa mwanafunzi katika kukamilisha kazi/shughuli mahususi. Wanafunzi watatathminiwa katika:
     - Kusoma - Madarasa ya 3-8 na 10

- Hisabati - Madarasa ya 3-8 na 10
- Sayansi - Madarasa ya 4, 7 na 11
- Mafunzo ya Jamii - Madarasa ya 5 na 8
- Kuandika - Madarasa ya 5, 8 na 11

- ARC hujaza Zana ya Tathmini ya Mpito ili kupima utendaji wa mwanafunzi katika stadi za masomo zinazohitajika kwa mpito. Wanafunzi watatathminiwa katika kusoma (Kiingereza na kusoma pamoja), hisabati na ujuzi wa sayansi katika darasa la 11.

**4. Je, nani huamua ikiwa mtoto wangu atafanya tathmini mbadala?**

ARC hufanya maamuzi kuhusu mpango wa elimu na mahali ambapo wanafunzi wenye ulemavu watawekwa. ARC pia itabaini jinsi wanafunzi wenye ulemavu wanavyoshiriki katika tathmini ya jimbo na wilaya. ARC hubaini ikiwa mwanafunzi atashiriki katika tathmini ya jimbo zima kwa marekebisho, bila marekebisho au ikiwa wanahitaji kutathminiwa kupitia tathmini mbadala.

**5. Je, ARC hufanya maamuzi vipi?**

Kwa kutumia Fomu ya Taarifa ya Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky, ARC itachambua taarifa ya mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na data ya maendeleo inayoendelea inayohusu kiwango cha sasa cha utendaji wa mwanafunzi. Miongozo ina vigezo vya kushiriki vinavyoelezea vipengele na sifa mahususi vya mafundisho. ARC lazima ijadili na ikubali kwa kusema "ndiyo" na itoe hati zinazohitajika kwa kila kigezo kutoka kwa miongozo ili kubaini ikiwa mwanafunzi anastahiki kushiriki katika tathmini mbadala. ARC lazima iwe na data mahususi ya uthibitisho na sababu ya kujibu "ndiyo" katika kila kauli, ikiwa ni pamoja na, bali si tu ripoti jumuishi ya elimu ya kisaikolojia, vipimo vya uwezo wa kufanya shughuli za kila siku, tathmini za mtaala, tathmini za utambuzi, ufuatiliaji wa maendeleo na kazi ya mwanafunzi.

**6. Je, ARC hufanya uamuzi wakati gani?**

ARC hukutana angalau kila mwaka ili kuchunguza mpango wa elimu wa mwanafunzi kwa kukagua na kurekebisha Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi (Individual Education Program (IEP)) wa mwanafunzi na kubaini jinsi ambavyo mwanafunzi atashiriki katika tathmini ya jimbo zima la Kentucky. Kwa kutumia Fomu ya Taarifa ya Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky, lazima ARC ikague na ibaini tena ikiwa mwanafunzi atashiriki katika tathmini mbadala kila mwaka.

**7. ARC ikishabaini kuwa mwanafunzi anastahiki kushiriki katika tathmini mbadala, je, huo ni uamuzi wa mwisho?**

Kulingana na data ya wakati ambapo ARC inakutana, huenda ikabainika kuwa mwanafunzi atashiriki katika tathmini mbadala. Data mpya ikijitokeza au kukiwa na mabadiliko, basi

huenda ARC ikakutana tena na kubaini kuwa mwanafunzi hastahiki tena kushiriki katika tathmini mbadala. Mkutano wa kila mwaka unaofanywa na ARC unapaswa kusaidia ARC kufanya uamuzi huo baada ya kila mwaka.

8. **Kwa nini mtoto wangu anafunzwa kwa kutumia maudhui sawa na watoto ambao hawana ulemavu? Ikiwa mtoto wangu anaweza kujifunza kwa mbinu hiyo, mbona elimu maalum inahitajika?**

   "ESSA [Sheria ya Kuhakikisha kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu] inahitaji wanafunzi wote wazingatie maudhui sawa ya masomo na viwango vya kufaulu (isipokuwa viwango mbadala vya kufaulu katika masomo kwa wanafunzi wenye ulemavu mkubwa zaidi wa utambuzi wa akili)." ESSA inahitaji kwamba tathmini mbadala zizingatie viwango vya maudhui ya ngazi darasa. (ESSA: Kanuni Kuu na Athari kwa Wanafunzi wenye Ulemavu)

9. **Kwa nini lazima mtoto wangu atathminiwe kwa kuzingatia viwango sawa vya ngazi ya darasa na wanafunzi ambao hawana ulemavu uliotambuliwa?**

   Kuna sheria mbili za shirikisho ambazo zinaamua jinsi shule zitawajibika kwa elimu ya wanafunzi wote nchini Marekani, ESSA na Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (IDEA 2004). ESSA na IDEA zina matarajio makubwa ya mafundisho na uwezo wa kujifunza kwa kutumia mtaala wa jumla kwa kila mtoto. Hii inahakikisha kwamba wanafunzi wote wanathaminiwa na wanaweza kujifunza katika viwango vya juu. Matokeo ya utafiti wa hivi majuzi yanaonyesha kuwa wanafunzi wenye ulemavu mkubwa wa utambuzi wa akili wanaweza kujifunza. Taarifa ya tathmini ya jimbo hutumiwa kusaidia katika kuboresha shule na mipango na kutoa uzoefu bora wa elimu kwa wanafunzi wote.

   Taarifa Zaidi:

   Mafundisho ya viwango vya maudhui ya ngazi ya darasa humpa mwanafunzi fursa ya kujifunza dhana ambazo anaweza kutumia katika hali nyingi na kujifunza stadi za utendaji wa shughuli za kawaida (maisha). Mchanganyiko wa fursa hizi mbili humsaidia mwanafunzi kuwa na uzoefu wa mzuri. Kwa mfano, wakati mwanafunzi anafanya shughuli ya kiwango kinachoomba wanafunzi wachambue data, wachore grafu na wachague majibu sahihi kwa kutumia data au grafu, mwanafunzi anaweza:

   - Kukuza zaidi stadi za mawasiliano na kijamii (ikiwa ni pamoja na swichi na Vifaa Mbadala vya Mawasiliano) wakati wa kufanya utafiti wa kukusanya data;
   - Kuimarisha uwezo wa kufikiria kwa umakini kuhusu nambari anapoingiza data kwenye grafu (kwa mfano, ujuzi wa hisabati wa kuhesabu vitu vingi kwa kugusa kila moja mara moja tu);
   - Kuongeza stadi za kufanya maamuzi sahihi na ya baada ya kuarifiwa anapotumia data kuchagua kwa kutumia data au grafu (kwa mfano, gani ina nyingi zaidi); na/au,
   - Kuongeza stadi anazoweza kutumia kazini (kwa mfano, kuingiza data kwenye kompyuta, kutumia swichi kuingiza data, kuhesabu watu katika duka kubwa).

Wanafunzi wanaofanya tathmini mbadala huruhusiwa kupata usaidizi ambao huwasaidia kujifunza na kujitegemea. Huenda usaidizi huu ukajumuisha kupunguza kiwango cha ugumu, kutoa picha au vitu na kutumia teknolojia ya kusaidia.

**10. Je, IEP ya mtoto wangu hubainisha mafunzo anayojifunza shuleni?**

Lengo la IEP ni kuhakikisha kuwa mtoto wako mwenye ulemavu anapata elimu ya umma inayofaa bure (free and appropriate public education (FAPE)). IEP ni mpango ulioandikwa unaoelezea mafundisho yaliyoundwa kwa njia maalum (specially designed instruction (SDI)), marekebisho/mabadiliko na huduma zinazohusiana zinazohitajika ili kushughulikia mahitaji ya mtu binafsi ya mtoto wako. SDI inafafanuliwa katika IDEA kama kubadilisha maudhui, mbinu au mbinu ya mafundisho kulingana na hali husika ili kushughulikia mahitaji ya kipekee ya mtoto na kuhakikisha kuwa anweza kujifunza kwa kutumia mtaala wa jumla ili mtoto aweze kufikia viwango vya elimu vya eneo la shirika la umma linalohusu watoto wote. (34 Sehemu ya CFR 300.39) Viwango vya elimu huko Kentucky ni KAS. Mwanafunzi anapofundishwa kila siku kwa kuzingatia viwango hivi vya maudhui darasani, vipengele vya IEP vilivyofafanuliwa wazi (kwa mfano, kiwango cha sasa cha utendaji, malengo ya kila mwaka na malengo/vigezo, marekebisho/mabadiliko) ni muhimu ili kuhakikisha kuwa anapata elimu inayofaa.

Taarifa Zaidi:

IEP haikusudiwi kuwa mpango mzima wa elimu wa mwanafunzi. Badala yake, ni mpango wa usaidizi ambao wanafunzi wanahitaji kupata ili kuhakikisha kuwa wanafanya maendeleo katika mtaala wa jumla. IEP hutengenezwa na ARC kama kumbukumbu ya maamuzi ambayo wanachama wake walifanya. IEP ni mpango wa utekelezaji na ahadi ya kuzingatia rasilimali zilizotambuliwa katika mpango. IEP inapaswa kubaini elimu maalum na huduma zinazohusiana na usaidizi ambao mwanafunzi anahitaji anapojifunza maudhui ya mtaala wa jumla.

**11. Je, tathmini mbadala hupunguza msaada ambao mtoto wangu anapokea?**

Mwalimu anapaswa kumpa mwanafunzi msaada anaohitaji ili ajifunze stadi zinazohitajika katika mtaala. Hata hivyo, mafundisho hayo yanapaswa kurekebishwa baada ya muda ili kumsaidia mwanafunzi kuweza kujitegemea kwa kiwango kikubwa ili wakati wa tathmini, mwanafunzi aweze kufanya kazi kwa kujitegemea kwa kiwango kikubwa kadri iwezekanavyo.

Taarifa Zaidi:

Usaidizi ambao mwanafunzi anapata wakati wa tathmini unapaswa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi binafsi. Usaidizi ambao mwanafunzi anapewa haupaswi kumwelekeza kwa jibu sahihi.

**12. Je, mtoto wangu anaruhusiwa kufanyiwa mabadiliko yoyote katika tathmini mbadala?**

Tathmini mbadala huwaruhusu wanafunzi kutumia usaidizi (mabadiliko, kubadilishiwa mafundisho na teknolojia ya kusaidia) wakati wa mafundisho na tathmini. Kutoa usaidizi huu humruhusu mwanafunzi kujifunza maudhui yanayolingana na umri wake, ya kuvutia na yanayomsaidia kukuza ujuzi mpya. Mabadiliko hayaruhusiwi ikiwa usaidizi huo utamwongoza mwanafunzi moja kwa moja kwa jibu sahihi. Mfano wa usaidizi unaoruhusiwa ni msimbo wa rangi, ili mwanafunzi ajue kuwa anapaswa kuanza na rangi ya kijani na kumaliza na nyekundu. Mfano wa usaidizi ambao hauruhusiwi ni kuandika jibu sahihi kwa rangi ya kijani na jibu lisilo sahihi kwa rangi nyekundu. Tarifa zaidi juu ya mabadiliko yanayoruhusiwa yamebainishwa katika Mipango ya Ujumuishwaji wa Watu Wanaohitaji Huduma Maalum Katika Tathmini Inayohitajika na Jimbo na Uwajibikaji 703 KAR 5:070.

Taarifa Zaidi:

Tathmini ya jimbo ya jumla pia huruhusu wanafunzi kutumia usaidizi wakati wa mafundisho na tathmini. Ili kutoa sababu inayokubalika ya kufanya marekebisho katika mitihani yoyote iliyoamuriwa na jimbo, marekebisho ya mitihani lazima yajumuishwe mara kwa mara kama sehemu ya mafundisho ya kawaida na tathmini ya darasa na pia kukidhi mahitaji yote ya ziada yaliyoanzishwa na Mipango ya Ujumuishaji wa Watu Wanaohitaji Huduma Maalum Katika Tathmini Inayohitajika nad Jimbo na Uwajibikaji 703 KAR 5:070.

**13. Je, marekebisho ambayo mwanafunzi wangu atafanyiwa kwenye tathmini mbadala huamuliwa vipi?**

ARC lazima ibaini marekebisho yanayohitajika kulingana na mahitaji ya mwanafunzi wako binafsi. Marekebisho hufanywa kwenye tathmini ili alama ya mtoto wako iakisi alichojifunza katika mtaala wa jumla.
Lazima marekebisho yahusiane na ulemavu wa mtoto wako, na kuwe na uthibitisho wa data ya tathmini. Lazima yaandikwe kwenye IEP na kutumiwa kama sehemu ya utaratibu wa kawaida wa mafundisho. Marekebisho hayawezi kutumiwa kwa madhumuni ya mitihani pekee. IEP lazima iandikwe ili kumsaidia mtoto wako kukuza stadi anazohitaji ili afaulu akijifunza kwa kutumia mtaala wa jumla, kwa hivyo marekebisho huamuliwa kila mwaka. Kadri mtoto wako anavyoimarisha stadi zake, ndivyo tunavyoweza kupunguza marekebisho mahususi.

Kwa mfano, mtoto aliye na ulemavu anayehitaji kusomewa nyenzo za ngazi ya darasa kwa sauti kubwa, baada ya muda, anaweza kukuza stadi za kusoma kwa kiwango ambacho huduma ya msomaji zitapunguzwa katika tathmini fulani na kusitishwa.
Marekebisho hayakusudiwa kuchukua nafasi ya mafundisho au matumizi ya teknolojia ya kusaidia. Kwa kuandika IEP, ARC inaweza kujadili njia za kupunguza matumizi ya marekebisho kwa muda. IEP itajumuisha taarifa inayoelezea marekebisho yoyote ambayo mtoto wako atatumia katika mitihani ya jimbo na wilaya nzima.

Taarifa Zaidi:

Unaweza kupata taarifa zaidi juu ya hali za jumla za kutumia marekebisho katika tathmini za jimbo kwenye ukurasa wa wavuti wa Tathmini Mbadala wa Kentucky .

**14. Je, mtoto wangu anaweza kupata cheti cha kawaida cha shule ya upili akifanya tathmini mbadala?**

ARC lazima ibaini ikiwa uwezo wa mwanafunzi wa utambuzi wa akili na uwezo wa kufanya shughuli za kila siku unamzuia kukamilisha kozi ya elimu ya jumla (ikiwa ni pamoja na mahitaji ya chini zaidi ya kuhitimu) hata kwa mabadiliko ya mpango na/au marekebisho. ARC hufanya uamuzi huu kwa kutumia data na taarifa mbalimbali kama vile Fomu ya Taarifa ya Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky, ripoti iliyojumuishwa ya elimu ya kisaikolojia, Zana ya Sifa za Wanafunzi Learner Characteristics Inventory (LCI)), kazi ya mwanafunzi, uchunguzi wa mwanafunzi na taarifa nyingine yoyote inayofaa. Ikiwa hii ndio hali, ARC lazima ibaini kuwa mwanafunzi hataweza kukamilisha kozi ya elimu ya jumla ili aweze kupata cheti cha kawaida cha shule ya upili na kwa hivyo atahitaji kukamilisha kozi mbadala ya kujifunza ili aweze kupata Cheti Mbadala cha Shule ya Upili kama ilivyoelezwa katika kanuni ya Kentucky ya 704 KAR 3:305, Sehemu ya 10.

Taarifa Zaidi:

Kushiriki katika tathmini mbadala hakumzuii mwanafunzi mwenye ulemavu mkubwa wa utambuzi wa akili kujaribu kukamilisha mahitaji ya kupata cheti cha kawaida cha shule ya upili kama ilivyoelezwa katika IDEA Kushiriki katika Tathmini (34 CFR§300.160 (d)(2)).

Unaweza kupata taarifa kuhusu mahitaji ya kuhitimu kwenye ukurasa wa wavuti wa Mahitaji ya Chini Zaidi ya Kuhitimu Kutoka Shule ya Upili .

**15. Je, mtoto wangu atajifunza lini kuhusu stadi za kusaidia watu kufanikiwa (za maisha) zilizoorodheshwa katika IEP?**

Walimu wote wanapaswa kuzingatia jinsi ambavyo mwanafunzi atatumia stadi zote alizojifunza. Hii ni kweli hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu mkubwa wa utambuzi wa akili. Stadi za maisha zinaweza kujumuishwa katika mafundisho. Ikiwa mwanfunzi hawezi kufundishwa stadi ya IEP darasani, basi wakati unapaswa kutengwa ili afunzwe stadi hiyo kama inavyohitajika. Baada ya mwanafunzi kukamilisha tathmini mbadala ya jimbo inayohitajika katika darasa la 12, basi mwanafunzi anaweza kuzingatia tu mpito wa kukuza stadi za maisha hadi umri wa miaka 21.

Taarifa Zaidi:

Kufuatia viwango vya ngazi ya darasa ambavyo vimeundwa kwa ajili ya wanafunzi wote ili kusaidia kuhakikisha kuwa mwanafunzi anafunzwa stadi mahususi wakati mwanafunzi anahama kutoka shule ya msingi hadi shule ya kati na kuendelea hadi shule ya upili, waalimu wanaweza kubinafsisha mafundisho na matarajio ili

kukidhi mahitaji ya mwanafunzi huku wakizingatia mtaala. Walimu wanapobinafsisha mafundisho na matarajio, wanaweza kusisitiza stadi za maisha na za IEP. Kwa mfano, wakati mwanafunzi wa shule ya msingi anajifunza kuhusu vipimo vya vimiminivu, mwanafunzi anaweza kujifunza kupima vimiminivu vya kupika au kufua. Wakati wanafunzi wa darasa la shule ya kati wanajifunza kuhusu hadithi za kubuni na za ukweli, mwanafunzi anaweza kujifunza kutambua nyenzo zenye taarifa ya ukweli (kwa mfano, vitabu vya kupika, magazeti, nk) na hadithi za kubuni (riwaya kwenye kinasa sauti). Wakati wanafunzi wa shule ya upili wanajifunza kuhusu utendaji wa kemikali, mwanafunzi anaweza kuzingatia kemikali za nyumbani anazopaswa kuepuka kuchanganya.

16. **Je, nini hufanyika ikibainika kuwa mtoto wangu anahitaji kubaki katika darasa kwa zaidi ya mwaka mmoja?**

    Lazima mwanafunzi aandikishwe tena katika darasa hilo kwenye kumbukumbu za shule na ashiriki katika tathmini mbadala ya ngazi ya darasa hilo tena. [703 KAR 5:240, Sehemu ya 8 (3)]

    Taarifa Zaidi:

    Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu wanafunzi wenye ulemavu kukosa kwenda katika darasa linalofuata katika barua ya Agosti 19, 2003 kutoka kwa Ofisi ya Elimu Maalum na Huduma za Kurekebisha Tabia (Office of Special Education and Rehabilitative Services OSERS)).

17. **Ninaweza kupata wapi taarifa zaidi kuhusu Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky?**

    Unaweza kupata mwongozo zaidi kuhusuFomu ya Taaarifa ya Miongozo ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky kwenye hati ya Mwongozo wa Kamati za Uandikishaji na Ukaguzi (Admissions and Release Committees (ARCs)) kuhusu Maamuzi ya Kushiriki katika Tathmini Mbadala ya Kentucky inayopatikana kwenye ukurasa wa Mwongozo wa Kushiriki .